2015[3], shirika hili linatambua umuhimu wa lugha ya kufundishia shuleni katika kukuza ubora wa kufundisha na kujifunza. Ripoti hii inaonyesha kuwa, mbali na lugha za kimataifa, lugha za kiasili zimetekeleza wajibu muhimu katika upatikanaji wa elimu, hasa kwa makundi madogo ya watu wanaoongea lugha zisizo maarufu.

Kwa mujibu wa Trudgil (1983), lugha ni chombo cha kubadilisha maadili, mielekeo na matarajio ya watu walio na utamaduni unaowatambulisha. Tukizingatia wazo hili, lugha za Kiafrika zina nafasi muhimu ya kuendeleza maadili na kubadilisha mielekeo na matarajio ya vijana kuhusiana na tamaduni, mataifa yao na bara la Afrika kwa jumla. Hili litawezekana pale lugha hizi zinatumiwa katika miktadha mbalimbali, ukiwemo muktadha wa elimu. Ni muhimu kutaja hapa kuwa kuna aina mbili za elimu – elimu isiyo rasmi (inayotokana na utangamano na mazingira) na elimu rasmi (inayotolewa shuleni na taasisi nyinginezo).

Lugha za Kiafrika ni chombo muhimu cha kuwasilisha turathi na falsafa za Kiafrika. Ili elimu iwafaidi walengwa panafaa kuwepo na uwiano kati ya elimu inayotolewa na lugha ya utamaduni wa wahusika (Wa Thiong'o, 1986). Mtaalamu huyu anashikilia kuwa lugha sio tu chombo cha mawasiliano bali pia ni chombo cha kubebea utamaduni. Elimu inayoendelezwa kwa lugha za kigeni haiwezi kuakisi mazingira halisi ya kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi ya mpokezi wake. Mwananchi aliyepagazwa elimu ya aina hii atakumbwa na changamoto chungu nzima atakapojaribu kuitumikiza maishani. Kwa mtazamo huu, elimu haiwezi kuwa chombo cha kuendeleza maendeleo endelevu iwapo itaurutubisha utamaduni wa kigeni unaowakanganya walengwa.

Kaviti na Ngugi (2016) wanasema kuwa lugha ni chombo muhimu cha kuiwezesha jamii kujitambulisha na kujibainisha na jamii zile zingine mbali na kuwawezesha wanajamii kuelewana na wenzao. Wataalamu hawa wanasisitiza umuhimu wa kufanya utafiti na kuandika kwa lugha za Kiafrika ili zisije kuangamia. Mawazo haya yanaungwa mkono na nadharia ya Utambulisho wa Jamii iliyoasisiwa na Tajfel na Turner (1979). Nadharia hii huiangalia jamii kwa misingi kama vile lugha, tamaduni, siasa, uchumi na biashara na jinsi wanajamii hujitambulisha kwa misingi hiyo. Kati ya misingi iliyotajwa hapa, lugha ndiyo gundi inayowaunganisha wanajamii kwani ndicho kipengele muhimu kinachotumiwa katika kuendeleza utamaduni, siasa, uchumi na biashara.

**Habari na Mawasiliano**

Vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kurahisisha biashara ya kisasa kwani pembe mbalimbali za ulimwengu zimeunganishwa kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (M'Ngaruthi, 2019). Kuibuka kwa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili kumechangia pakubwa katika maendeleo ya sehemu za mashambani (Wasike, 2019). Kwa mujibu wa Tume ya Mawasiliano ya Kenya, kuna vituo thelathini vinavyotangaza kwa lugha za kiasili (mbali na Kiswahili) nchini Kenya. Vituo hivi vimesambaa katika maeneo ya miji na mashambani na huwafikia wasikilizaji wake katika kaunti zote nchini. Kwa mfano, wasikilizaji wa lugha ya Kimeru nchini Kenya wana vituo vya redio kama vile Muuga FM, Meru FM, Mwago FM, Wega FM, Weru FM, Geetu FM na Mwariama FM. Isitoshe, kuna vituo vya runinga kama vile Mwariama Tv, Weru Tv, Baite Tv na Meru Tv ambavyo hutoa matangazo yake kwa lugha iyo hiyo.

Umaarufu wa vyombo hivi umedhihirika hasa katika maeneo ya mashambani kwani vipindi vyake hutoa burudani na mafunzo muhimu kwa lugha zinazoeleweka na wengi. Idhaa nyingi huinufaisha hadhira yake katika masuala ya elimu, siasa, utamaduni, mazingira, dini na afya. Kwa mfano, kipindi cha 'Murimi Caruruku' (Mkulima Shupavu) kwenye Weru Tv huwashirikisha wakulima na wafugaji katika majadiliano kuhusiana na ufanisi na changamoto wanazopitia katika shughuli zao. Wakulima na washikadau wengine katika sekta hiyo pia hupata fursa ya kuuliza maswali na kushauriwa na wataalamu wa kilimo.

Vyombo hivi vya habari pia huwa katika mstari wa mbele kuufahamisha umma kuhusu kuzuka kwa majanga mbalimbali. Kwa mfano, vyombo hivi vilichukua hatua muhimu katika kuuangazia umma kuhusu uvamizi wa nzige katika maeneo kadha nchini Kenya mwanzoni mwa mwaka wa 2020. Ni vyombo vivyo hivyo vilivyotumiwa na serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuuelimisha umma juu ya jinsi ya kuwakabili wadudu hao waharibifu ambao tayari walikuwa wameyaharibu maelfu ya tani za chakula. Habari za mafuriko yaliyosababisha maafa makubwa katika maeneo mbalimbali nchini Kenya mwaka wa 2019 na 2020 ziliangaziwa katika idhaa nyingi zinazotangaza kwa Kiswahili na lugha nyinginezo za wenyeji.

Licha ya hatua muhimu zilizoshuhudiwa, ongezeko la vituo hivi limesababisha utashi mkubwa wa waandishi wa habari, wahariri na watangazaji walio na ujuzi wa lugha husika. Inasikitisha kuona kuwa waandishi wengi wa habari, wahariri, watangazaji na waandalizi wa vipindi vya redio na runinga hawana ujuzi wa lugha walizoajiriwa kuendeleza. Wengi wao ni vijana wasio na ujuzi wowote wa lugha hizi. Baadhi yao wanapozungumza huwafedhehi waajiri wao kutokana

[3] Tazama Ripoti ya UNESCO – Elimu kwa Wote: Mafanikio na Changamoto kupitia www.efareport.unesco.org

na matumizi mabovu ya lugha, ikiwa ni pamoja na kuchanganya lugha mbalimbali wanapotangaza.

Sekta hii pia inakumbwa na changamoto kubwa ya utafsiri wa habari kutoka lugha moja hadi nyingine. Hali hii inaathiri usambazaji wa habari sahihi kwani baadhi ya watafsiri huupotosha ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano, habari muhimu kuhusiana na majanga kama vile mafuriko, kuenea kwa nzige na usambaaji wa maradhi hatari ya korona zisipotafsiriwa ipasavyo zinaweza kuwatia wananchi hatarini. Isitoshe, huenda habari muhimu zikapotea kabisa wakati wa utafsiri. Sera za serikali na habari nyingine muhimu zisipowafikia wananchi kama zilivyokusudiwa bara hili litaendelea kubaki nyuma katika utekelezaji wa mipango muhimu ya serikali. Ujumbe uliopotoshwa katika tafsiri pia unaweza kuzua taharuki miongoni mwa wanajamii na kuugawanya umma kwa misingi ya kikabila, kidini au kitabaka.

**Tafsiri na Ukalimani**

Kuna aina mbalimbali za tafsiri. Hizi ni pamoja na tafsiri ya makala, tafsiri ya mtandao, tafsiri ya vitandazi, tafsiri ya filamu, ukalimani andamizi, ukalimani mtawalia, ukalimani wa simu, ukalimani kupitia video, ukalimani wa lughaishara, ujanibishaji, ufundishaji wa lugha, uandishi wa vitabu vya lugha, sanaa ya lugha, uhariri, uundaji wa istilahi, utafiti wa lugha, pamoja na uundaji na uuzaji wa nyenzo za kielektroniki za kutafsiria (Kamundi, 2019).

Wakalimani na watafsiri wanahitajika katika sekta nyingi, ikiwa ni pamoja na tafsiri za moja kwa moja au kupitia vyombo vya kielektroniki. Baadhi ya nchi za Kiafrika zimepiga hatua za kufundisha masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa lugha za kiasili (Kevogo, 2018). Hatua hii imewezeshwa na juhudi za wataalamu za kufanya utafiti na kutafsiri istilahi za kiteknolojia kwa lugha za kiasili. Bila shaka juhudi hii imezaa matunda kwani imeibua kizazi kipya kinachoweza kuendeleza maarifa haya kwa vizazi vijavyo kwa lugha wanayoielewa kwa urahisi.

Ukalimani katika makongamano ya kimataifa ambapo washiriki wake huwa wasemaji wa lugha ainati umekuwa maarufu kote ulimwenguni. Aidha, wakalimani huhitajika katika mikutano ya kidini ili kuwawezesha walengwa kupokea ujumbe kwa urahisi. Watafsiri wa vitabu, makala, habari na matangazo katika vyombo vya habari wanahitajika kote ulimwenguni.

**Sekta ya Dini**

Kwa mujibu wa Kevogo, Mukuthuria na Mukhwana (2015), usemi wa kidini ni usemi wa kijamii unaoshirikisha wahubiri na waumini wao ambao hutangamana na kuwasiliana wakitumia lugha. Wataalamu hawa wanasema kuwa mawasiliano ya kidini yanapaswa kutumia lugha kwa uangalifu ili kuwashawishi na kuwaathiri waumini kufikiri, kutenda na kubadili mitazamo yao ya kilimwengu kwa njia inayoafiki matarajio mema ya jamii. Wanaonya pia kuwa iwapo usemi utatumiwa vibaya unaweza kuwa hatari na kuzua chuki. Hii inamaanisha kuwa pana haja ya wahubiri kuwa na msingi mwema wa lugha utakaowawezesha kuitumia kwa upole na kuzingatia miktadha ifaayo ili kutekeleza wajibu huu muhimu.

Hali ilivyo hivi sasa ni kwamba pana wahubiri wengi wasio na ujuzi wa kusoma na kufasiri maandiko matakatifu kwa Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Hata wanapokuwa na ujuzi huu, wahubiri wengi wa kisasa hupenda kutumia lugha za kigeni, hasa Kiingereza. Hapa ndipo panapohitajika wakalimani na watafsiri wenye ujuzi wa lugha hizo za kigeni pamoja na lugha za kiasili ili kuwawezesha wenyeji kulipata neno la Mungu kwa njia mwafaka. Hii ni kwa sababu kazi nzuri ya tafsiri inafaa kuzingatia utamaduni wa lugha chanzi na lugha lengwa (Malangwa, 2017).

Wahubiri pia wana jukumu la kuielimisha jamii kuhusiana na masuala-ibuka kama vile athari za mafuriko, uharibifu wa mazingira na maradhi hatari ya korona. Nchini Kenya pamekuwepo na visa vya wahubiri wachache waliojaribu kuwapotosha wananchi kuhusiana na hali halisi ya maradhi hayo. Madhalani, mhubiri mmoja kutoka kwa kanisa la kibinafsi mjini Meru aliripotiwa katika vyombo vya habari akiwaambia wafuasi wake kuwa hakukuwa na ugonjwa kama korona. Jijini Nairobi mhubiri mmoja maarufu alidai kuwa angewaponya wagonjwa wa korona kwa kuwachezea gitaa na kuimba nyimbo za sifa. Kwa kuwa viongozi wa kidini wana ushawishi mkubwa miongoni mwa wanajamii, ujumbe wa kiupotoshi kama huu, hasa unapotolewa kwa lugha za kiasili katika maabadi ya vijijini, unaweza kuzua taharuki kuu. Hali hii huenda ikaufanya umma kuzikaidi juhudi za serikali za kupambana na changamoto nyingi zinazolikumba taifa na ulimwengu kwa jumla.

**Uandishi na Uchapishaji**

Nafasi ya sekta ya uandishi na uchapishaji katika uendelezaji wa elimu haiwezi kupuuzwa katika ulimwengu uliostaarabika. Mamilioni ya tani za machapisho hutolewa kila mwaka ili kukidhi mahitaji ya maandishi katika viwango mbalimbali vya elimu. Kabla ya kuwafikia wasomaji wake, machapisho haya hupitia mchakato changamano wa uwazaji, uandishi, uhariri na uchapishaji. Iwapo mchakato huu utaingia dosari katika kiwango cha uandishi, kazi itakayoibuka itakuwa chapwa kiasi cha kutokuwa na maana yoyote kwa msomaji. Matumizi yake katika viwango mbalimbali vya elimu hatimaye yataathiri utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu.

Kati ya vigezo vinavyozingatiwa katika maandalizi ya kitabu ni utamaduni wa wasomaji, umri

wao, viwango vya elimu na mazingira wanamopatikana. Vigezo hivi ndivyo humwongoza mwandishi katika kuteua lugha atakayotumia katika kazi yake. Kama anavyosisitiza Wa Thiong'o (1986), lugha ya elimu inayo dhima kuu ya kuwasilisha na kuhifadhi utamaduni na turathi za jamii yoyote. Kazi inayolenga kiwango chochote cha elimu sharti iakisi uhalisi wa jamii husika. Katika muktadha huu, mwandishi anapaswa kuwa na ufahamu wa kina kuhusiana na hadhira anayonuia kuandikia kabla hajaanza uandishi wake. Isitoshe, mwandishi anafaa kuwa na ufahamu wa lugha anayonuia kutumia.

Mchakato wa uandishi pia huhitaji wahariri walio na ujuzi wa lugha iliyotumika. Mhariri ndiye huifanya kazi inayohusika kuchukua muundo unaohitajika pamoja na kuhakikisha habari sahihi zinachapishwa. Udhaifu wa kiuhariri huifanya kazi hiyo kuwa na makosa mengi ya lugha na usahihi wa habari. Hali hii inaweza kuharibu sifa ya shirika la uchapishaji na hata mwandishi mwenyewe na pia kuwapotosha wasomaji. Makosa mengi ya aina hii hujitokeza katika vitabu, magazeti na majarida iwapo wahariri hawakumakinika katika lugha za kazi wanazohariri.

Mabadiliko yaliyopendekezwa katika Mtaala wa Kiumilisi nchini Kenya yananuiwa kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Vitabu vingi vilivyoandikwa kwa lugha za wenyeji vitahitajika ili vitumike katika shule za msingi zilizo katika maeneo ya mashambani kwani kila Mkenya ana uhuru wa kutumia na kudumisha lugha pamoja na utamaduni wake (Katiba ya Jamhuri ya Kenya, 2010, 44(33). Ufunzaji wa lugha ya Kiswahili pia umetiliwa mkazo katika shule zilizoko mijini. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala nchini Kenya imeshachukua hatua ya kuwaandalia warsha waandishi wa vitabu vya lugha mbalimbali za kienyeji nchi Kenya.

**Utafiti**

Lengo kuu la utafiti ni kupata suluhu kwa matatizo yanayoikumba jamii. Kupitia utafiti, utekelezeji wa malengo ya maendeleo endelevu kama vile upunguzaji wa vifo vya watoto na akina mama wajawazito na utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wote huafikiwa. Watafiti wanapogundua na kuvumbua mambo mapya wana jukumu la kuyafasiri na kuusambazia umma matokeo ya utafiti huo ili manufaa yake yawafikie walengwa. Kwa mfano, kuzuka kwa maradhi hatari ya korona kumewafanya watafiti kote ulimwengu kujitahidi ili kupata tiba na chanjo yake. Pamekuwepo na mjadala wa iwapo chanjo hiyo ifanyiwe mararibio barani Afrika au la. Mojawapo ya matatizo yaliyokinza hatua hii muhimu ya kiutafiti ni ukosefu wa mawasiliano mwafaka na wananchi wanaonuiwa kuhusishwa.

Bara la Afrika lina wasomi na watafiti wengi ambao hawawezi kuwasiliana na wanajamii kwa kutumia Kiswahili au lugha nyingine za wenyeji. Wengi wa wataalamu hawa hupenda kujifaharisha kwa matumizi ya istilahi ngumu za kitaaluma ambazo hazimnufaishi mwananchi wa kawaida. Wananchi wengi wanaoishi mashambani huwaajabia wasomi hawa wanaoonekana kuishi katika ulimwengu wa ndoto. Udhaifu huu umelifanya bara la Afrika kuwa na maarifa mengi yaliyogubikwa katika majarida ya kitaaluma na akilini mwa watafiti. Sekta zilizoathiriwa na usomi huu wa kinadharia ni pamoja na afya, kilimo, uhandisi na elimu. Pana haja ya wataalamu katika sekta mbalimbali kuwa na uwezo wa kimsingi wa lugha ya huduma na kuziacha istilahi za kitaaluma katika uwanja wa kiakademia.

**Sekta ya Afya**

Afya ya wananchi huchangia pakubwa katika maendeleo endelevu ya taifa lolote. Sehemu kubwa ya bajeti ya taifa hutengewa sekta ya afya kwani taifa lenye watu waliodhoofika kiafya ni taifa legevu katika utoaji huduma na uzalishaji mali. Mawasiliano mwafaka yana nafasi kubwa katika kuhakikisha utoaji bora wa huduma za afya. Miaka michache iliyopita pameshuhudiwa changamoto kubwa ambapo madaktari walioagizwa na serikali ya Kenya kutoka Cuba hawangeweza kuwasiliana na wagonjwa katika maeneo mbalimbali nchini. Utata huu ulitokana na ukweli kwamba asilimia kubwa ya Wakenya wanaoishi vijijini huwasiliana kwa lugha za kienyeji. Madaktari kutoka Cuba hawakufahamu lugha hizi kwani walizungumza Kiingereza na Kihispaniola. Hali hii iliifanya serikali kutumia pesa nyingi katika kuwaajiri wakalimani na kuwapa baadhi ya madaktari hao mafunzo ya kimsingi ya Kiswahili (Business Daily, Thursday, July 5, 2018).

Changamoto iliyojitokeza hapa inabainisha kuwa sekta ya afya inahitaji mawasiliano mwafaka ili kuhakikisha kuwa wagonjwa wanapata tiba ifaayo. Pana haja ya kuwa na wahudumu wa afya wanaoweza kuwasiliana kikamilifu na wananchi bila kuhitaji wakalimani. Utabibu unahitaji usahihi mkubwa katika utambuzi wa magonjwa ili huduma sahihi itolewe. Utata kidogo katika mawasiliano unaweza kumfanya daktari kutoa huduma isiyofaa, hali inayoweza kumuathiri mgonjwa, na wakati mwingine kusababisha kifo. Tunapostaajabishwa na kioja cha madaktari kutoka Cuba, tusije kamwe kupuuza ukweli kwamba tunao wahudumu wa Kiafrika wasioweza kuwasiliana hata kidogo kwa lugha za kiasili, kikiwemo Kiswahili.

Lugha za Kiafrika pia zinayo nafasi ya kuuhamasisha umma kuhusiana na masuala ya afya na lishe bora. Wataalamu wa sekta hii walio na ujuzi wa lugha hizi huchangia pakubwa wanapojadili mada mbalimbali kupitia kwa vyombo vya habari. Wananchi hufaidika pakubwa wanapopata fursa ya kutoa maoni yao na pia kuuliza maswali kwenye vipindi vya redio na runinga kwa lugha iliyo rahisi kwao.

**Janga la Korona**

Maradhi hatari ya Korona (Covid-19) yalipozuka nchini Uchina mnamo Novemba 2019 na kusambaa kwenye mataifa mengi ulimwenguni huku yakiwaathiri mamilioni ya watu, palihitajika njia mwafaka za kuuelimisha umma kuhusiana na janga hili. Vyombo vya habari vinavyotangaza kwa Kiswahili na lugha nyingine za kiasili viliwawezesha wananchi wengi, hasa wanaoishi katika maeneo ya mashambani, kufikiwa na habari kuhusiana na jinsi ulivyosambazwa, dalili zake na jinsi ya kujikinga nao. Aidha, palitolewa hamasisho kuhusiana na umuhimu wa kuchanjwa dhidi ya maradhi haya. Habari hizi zilisambazwa kupitia taarifa za habari, matangazo mahsusi pamoja na mbinu za sanaa kama vile nyimbo na maigizo mafupi.

Ni dhahiri kuwa taarifa za kila siku zilizotolewa na Wizara ya Afya nchini Kenya kuhusiana na idadi ya watu waliopimwa, walioambukizwa, waliopata nafuu na waliofariki pamoja na mikakati ya serikali ya kupambana na virusi hivyo zilikuwa katika lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, palikuwepo na nafuu kwa wananchi wengi waliokosa kuelewa Kiingereza kwani maelezo mafupi yalianza kutolewa kwa Kiswahili mwishoni mwa hotuba rasmi kutokana na malalamiko ya wanahabari wanaotangaza kwa Kiswahili. Aidha, vyombo vya habari vilihakikisha habari hizi ziliwafikia wananchi wengi iwezekanavyo kwa kuzitafsiri kwa Kiswahili na lugha nyingine za kiasili. Kwa upande mwingine, mashirika, viongozi pamoja na wananchi wa tabaka mbalimbali waliusambaza ujumbe huo katika mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter na Whatsapp kwa lugha zilizoeleweka kwa urahisi na hadhira yao.

**Sekta ya Kilimo**

Kwa kuwa bara la Afrika halijajimudu pakubwa katika sekta ya viwanda, kilimo huchukuliwa kuwa uti wa mgongo wa mataifa mengi. Sekta hii ndiyo hutegemewa na wananchi wengi kwa chakula na mapato. Kwa mfano, sekta hii huajiri asilimia 40 ya Wakenya wote na zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanaoishi maeneo ya mashambani. Aidha, nchi ya Kenya hupata asilimia 50 ya mapato kutoka nje ya taifa kutokana na mauzo ya mazao ya kilimo na bidhaa zake. Hali hii imelifanya bara hili kutumia rasilimali nyingi katika kuiendeleza sekta hii kupitia mafunzo na utafiti.

Wataalamu wa kilimo wanaotokana na juhudi hizi hutarajiwa kufanya kazi katika maeneo ya mashambani ambako shughuli za kilimo zimekita mizizi. Dhima kuu ya wataalamu hawa ni kutangamana na wakulima na washikadau wengine katika sekta hii ili kuwasaidia kuongeza mazao na kukabiliana na changamoto zozote zinazoweza kuhatarisha uzalishaji wa chakula na bidhaa nyinginezo. Wataalamu hawa hutarajiwa kuwasambazia wakulima maarifa yanayotokana na elimu na utafiti kama vile uvumbuzi wa mbegu mpya zinazoweza kukabiliana na hali mbalimbali za kimazingira. Hata hivyo, baadhi ya wataalamu hushindwa kutekeleza majukumu hayo ipasavyo kutokana na changamoto ya mawasiliano. Taaluma nyingi, ikiwemo ile ya kilimo, zimetawaliwa na watu waliofuzu kutoka kwa shule za kibinafsi na zile za kimataifa ambamo Kiingereza na lugha nyingine za kigeni hupewa kipaumbele. Inatazamiwa kuwa mtaala mpya wa elimu nchini Kenya ambao unasisitiza umilisi na utumikizi wa vipaji pamoja na ukuzaji wa lugha za kienyeji utasaidia kujaza pengo hili.

**Makazi na Usafiri**

Ajenda ya serikali ya Kenya ya kuwepo na makazi bora na kwa gharama ya chini inahitaji kupewa kipaumbele. Wakazi wengi wa maeneo ya vijijini na mitaani hawana makao bora na idadi ya watu wanaoishi katika maeneo ya mabanda inazidi kuongezeka (The Guardian, Thursday 28th March 2019). Isitoshe, makazi hayo yanapatikana katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi kutokana na barabara mbovu. Hali ilivyo hivi sasa ni kuwa taaluma ya uhandisi imekaliwa na wageni kutoka Uchina ambao hawawezi kuwasiliana na kushauriana ipasavyo na wawekezaji na wafanyikazi wa Kiafrika. Serikali za mataifa ya Kiafrika hazina budi kutafuta suluhu kwa changamoto hii kupitia kuwaandaa wahandisi wake wanaoweza kuelewana na wawekezaji na wafanyikazi ambao wengi ambao hawakubahatika kupata elimu ya juu.

**Utamaduni na Mazingira**

Lugha ni chombo muhimu katika uimarishaji wa utamaduni na mazingira, ambavyo udumishaji wake ni viakisi muhimu vya jamii yoyote inayoweza kudai kuwa na ustaarabu (M'Ngaruthi, 2019). Utamaduni na mazingira anayoishi mtu ndiyo humtambulisha na kumpa hadhi katika jamii. Iwapo masuala haya mawili yatapuuzwa, Waafrika watabaki kuwayawaya na kuyumbayumba kama ndege asiye na pa kutua. Pana haja ya kuwa na mikakati mwafaka ya kuhakikisha kwamba utambulisho huu muhimu unadumishwa kupitia elimu kwa umma. Lugha za kiasili ni muhimu kwani zina uwezo wa kuusawiri utamaduni na mazingira ya Mwafrika bila kupotoka. Lugha hizi zinafaa kutumiwa ili kuuhamasisha umma kuhusiana na umuhimu na mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa katika uhifadhi wa mazingira yanayozidi kuchafuliwa na ongezeko kubwa la watu, viwanda na magari kote ulimwenguni. Aidha, utamaduni unaweza kudumishwa kupitia tamasha mbalimbali zinazoendelezwa kwa lugha hizi. Elimu juu ya masuala haya pia inaweza kutolewa kupitia kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa lugha za wenyeji ili kuwafikia watu wengi iwezekanavyo.

**Hitimisho**

Imebainika katika makala hii kuwa kuna aina mbili za lugha kwa misingi ya utumikizaji wake – lugha za kitaaluma na lugha za huduma. Lugha za kigeni, ambazo hutumika katika taaluma mbalimbali,

zimegubika mengi kwenye uchangamano wa istilahi zake. Lugha hizi zilizojaa masuala ya kiakademia huenda zisimfaidi mwananchi wa kawaida. Lugha za kiasili, ikiwemo ile ya Kiswahili, hutekeleza wajibu muhimu katika utoaji wa huduma panapohitajika mawasiliano sahili. Lugha hizi ni muhimu kwani ndizo zinazowafikia watu wengi, hasa wanaoishi katika maeneo ya mashambani. Makala hii haipingi kamwe matumizi ya lugha za kigeni bali inapendekeza kuwepo kwa juhudi mahsusi za kuhakikisha kuwa habari zinawafikia wananchi kwa lugha wanayoielewa.

Uafikiaji wa ajenda na malengo mbalimbali ya maendeleo endelevu utagonga mwamba iwapo wananchi wanaopaswa kuyatekeleza hawataelewa wanachohitajika kufanya. Ujumbe muhimu kuhusiana na elimu, afya, siasa, dini, usalama na sera mbalimbali za serikali pia unapaswa kuwasilishwa kwa lugha ya mwananchi wa kawaida. Serikali Na waandalizi wa mitaala wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa Wakenya wote wanapata msingi bora wa lugha hizi. Mfumo wa elimu unaozipa kipaumbele lugha za kigeni na kudunisha Kiswahili na lugha za wenyeji hautatimiza lengo hili.

## MAREJELEO


- Akaka, L. (2017). Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya. Katika Kioo cha Lugha Juz. 11 (kur. 47-57)
- Business, Daily. (Thursday, July 5, 2018). Taxpayer burden in curing Cuban doctors' language problem. Imepakuliwa kutoka https://www.businessdailyafrica.com/news/counties/Taxpayer-burden in-curing Cuban doctors--language-problem/4003142-4648484-5j2ia2z/index.html.
- Kamundi, H.M. (2019). Biashara ya Huduma za Lugha: Mbona Bara la Afrika Linabaki Nyuma? Katika Kobia, J.; Kandagor, M. & Muita, L.C. (Wah.). Lugha na Fasihi katika Mshikamano wa Kitaifa na Uwiano Barani Afrika. (kur. 155-163).
- Katiba ya Jamhuri ya Kenya. (2010). Imepakuliwa kutoka http://www.coekenya.go.ke/2-1-2010
- Kaviti, F.M., & Ngugi, P. (2015). Mbinu za Kujiimarisha na Kujidumisha Kilugha kwa Wambeere. Katika Mukuthuria, M, Ontieri, J.O & Sanja, L. (Wah). Kiswahili na Maendeleo ya Jamii. Dar es Salaam: TUKI (kur. 211-220).
- Kevogo, S. A. (2018). Kiswahili katika Kufundishia TEHAMA katika Shule za Msingi nchini Tanzania: Umuhimu Na Changamoto Zake. Katika Kioo cha Lugha Juz. 13 (kur. 51-64).
- Kevogo, A. U., Mukuthuria, M., Mukhwana, A. (2018). Michakato Mipya ya Kueneza Dini Kiutandawazi na Athari zake katika Mustakabali wa Maenezi ya Kiswahili. Katika Omari, S., & Method, S. (Wah.). Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (kur. 549)
- Malangwa, P.S. (2017). Mchango, Maendeleo na Changamoto Zinazokabili Taaluma za Tafsiri na Ukalimani katika Kiswahili. Katika Kandagor, M.; Ogechi, N. & Vierke, C. (Wah.). Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja. Eldoret: Moi University Press (kur. 267-277).
- M'Ngaruthi, T.K. (2019). Dhima ya Kiswahili katika Uimarishaji wa Utamaduni na Mazingira kwa Mujibu wa Katiba ya Kenya. East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature, 2(9).
- M'Ngaruthi, T.K. (2019). Kiswahili na Uenezi wa Biashara katika Muktadha wa Utandawazi. Katika Walibora, K.W., Kipacha, A.H. & Simala, K.I. (Wah.) Kiswahili, Utangamano na Maendeleo Endelevu Afrika Mashariki. Zanzibar: KAKAMA (kur. 240-249). Simala, K.I. (2019). Dibaji. Katika Walibora, K.W., Kipacha, A.H. & Simala, K.I. (Wah.) Kiswahili, Utangamano Na Maendeleo Endelevu Afrika Mashariki. Zanzibar: KAKAMA (kur. viii-x).
- Tajfel, H., & Turner, J. C. (1979). An Integrative Theory of Intergroup Conflict: The Psychology of Intergroup Relations. Imepakuliwa kutoka https://www.simplypsychology.org/social identity-theory.html27-2018.
- The Guardian. (Thursday, March 28, 2019). Housing in Sub-Saharan Africa improves but millions of people live in slums. Imepakuliwa kutoka www.theguardian.com.
- Trudgil, P. (1983). Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society. England: Penguin Books.
- Wasike, M. (2019). Lugha za Kiasili Zinavyoathiri Matumizi ya Kiswahili: Uchunguzi waRedio za FM Zinazotumia Kibukusu katika Kaunti ya Bungoma. Katika Kobia, J.; Kandagor, M. & Muita, L.C. (Wah.). Lugha na Fasihi katika Mshikamano wa Kitaifa na Uwiano Barani Afrika (kur. 87-93).
- Wa, Thiong'o, N. (1986). Decolonising the Mind: The Politics of Language and African Literature. Nairobi: Heinemann Kenya.


**Cite This Article:** Timothy Kinoti M'Ngaruthi (2021). Mchango wa Lugha za Kiasili katika Uafikiaji wa Maendeleo Endelevu. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, 4(6), 242-247.